

e-Mrejesho yaipa Tanzania tuzo UN

Na Mwandishi Wetu

TANZANIA imeshinda tuzo ya Umoja wa Mataifa (UN) ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 kupitia mfumo wa

e-Mrejesho.

Tuzo hiyo ilitolewa katika hafla ya utoaji tuzo za UN Juni 26, mwaka huu kwenye kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa katika Jiji la Incheon, Jamhuri ya

Korea.

Mfumo wa e-Mrejesho umetambuliwa na UN kama jukwaa linaloweza shirika kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijiti na kufanya maamuzi ya sera

na utekelezaji kwa wakati.

Tanzania na Afrika Kusini ndio nchi pekee kutoka Afrika zilizotunukiwa tuzo hiyo, kati ya nchi 73 wanachama wa UN zilishiriki na mifumo 400 iliwasilishwa huku mifumo 15 ikishinda tuzo mbalimbali ukiwemo mfumo wa e-Mrejesho.

Tuzo hiyo iliypokelewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa UN katika Idara ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii, Li Junhua na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Korea, Lee Sang-Min.

Mfumo wa e-Mrejesho umesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaruhusu wananchi kuwasiliana na taasisi zote za serikali na kuwasilisha maoni, malalamiko au pongezi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba alisema tuzo hiyo inaonesha kutambuliwa kwa mchango wa mfumo huo duniani kama jukwaa huru linalowaunganisha wananchi na serikali katika kuboresha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

"Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa

huru kwani umezingatia faragha za wananchi ambapo kwa wale wasiopenda kujulikana wanapowasilisha maoni yao serikalini wanaweza kuwasilisha bila kujulikana, na hivyo kuhakikisha sauti za watu zote zinasikilizwa, hii inachochea utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma," alisema Ndomba.

Aliongeza kuwa, mfumo wa e-Mrejesho ni hatua kubwa katika juhudi za e-GA za kujenga daraja kati ya serikali na wananchi wake na kuwa ushindi wa tuzo hiyo kutoka kwa Umoja wa Mataifa unaonesha namna azma ya e-GA ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia inavyotekelezwa.

Mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kwa njia tatu ambazo ni kupitia simu ya mkononi kwa kubofya *152*00# kisha namba tisa halafu mbili, kupitia simu janja kwa kupakua App ya e-Mrejesho na kwa njia ya tovuti ya emrejesho.gov.go.tz.

Wiki ya Huduma ya Umma ya Umoja wa Mataifa ni tukio la kila mwaka linaloadhimishwa kimataifa kwa lengo la kusherehekea thamani na umuhimu wa huduma ya umma kwa jamii na hujadili jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma kwa umma duniani kote.

TSN TANGAZA MATANDAO YA KADIMBA

Punguzo la Saba saba

Tangaza na magazeti ya **Daily News** na **HabariLEO** na upate punguzo la asilimia 20 na zaidi kwa matangazo, makala na mitangazo yatakavyotoka katika Mjukwaa ya Kidijiti ya TSN. Pia, pata huduma za uchapaji wa kibishara kwa bidhaa chapishi kwa bei nafuu.

Wasitiana nasi leo, upate ofa hii
 Simu: +255 22 2116074 0713 598 567 0713 513 956
 Barua pepe: matangazo@tsn.go.tz

Uguzo wa maabara wa kazi

HabariLEO.tz
dailynews.tz

sproutled
Daily News
Tanzania
mhasani@tsn

mhasani@tsn
dailynews.tz

Daily News
Digital

DAILY NEWS | **sundaynews** | **HABARILEO** | **SPLO**